

KCU  
QUALITY  
COFFEE



*Kagera Cooperative Union*

Kumb.Na.KCU/M.1/V/1

06/04//2023

Wajumbe wa Mkutano Mkuu  
KCU (1990) Ltd,  
Chama cha Ushirika cha Msingi.....  
**BUKOBA (M), BUKOBA (V), MISSENYI NA MULEBA.**

**YAH: TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA CHAMA KIKUU CHA  
USHIRIKA KAGERA – KCU (1990) LTD UTAKAOFANYIKA TAREHE 28/04/2023  
KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO BUKOBA COOP. HOTEL.**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

Kwa mujibu wa kifungu cha 46(d) cha Masharti ya KCU (1990) Ltd, Mwenyekiti wa Bodi ya KCU (1990) Ltd anayo heshima kuwatangazia Mkutano Mkuu wa mwaka wa KCU (1990) Ltd utakaofanyika tarehe 28/04/2023, kuanzia saa tatu kamili asubuhi katika Ukumbi wa **BUKOBA COOP. HOTEL Bukoba Mjini.**


Agenda za Mkutano zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Kuchagua mwenyekiti wa Mkutano
2. Kufungua Mkutano Mkuu
3. Kusoma tangazo la Mkutano, kuridhia agenda na kuthibitisha Akidi.
4. Kusoma vifungu vya masharti vinavyohusu Mkutano Mkuu
5. Kujadili maombi ya chama kilicholeta maombi ya kujiunga na KCU.
6. Hotuba ya mgeni rasmi
7. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa thelathini na mbili wa mwaka uliofanyika tarehe 12/04/2022.
8. Yatokanayo na muhtasari wa Mkutano Mkuu wa thelathini na mbili wa mwaka uliofanyika tarehe 12/04/2022.

9. Kusoma na kujadili taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi
10. Kusoma na kujadili mizania ya KCU(1990) Ltd msimu 2021/2022.
11. Kusoma, kujadili na kupitisha makisio ya mapato na matumizi msimu 2023/2024.
12. Kujadili na kupitisha ukomo wa madeni msimu 2023/2024.
13. Kujadili na kupitisha sera za uendeshaji wa chama.
14. Kupitisha kamati za usimamizi wa fedha za ustawi wa jamii.
15. Mengineyo kwa ruhusa ya Mwenyekiti
16. Kufunga Mkutano

Kabla ya mkutano kuanza wajumbe watapata fursa ya kutembelea na kuona maendeleo ya ujenzi wa ukumbi wa mikutano uliopo katika viwanja vya Rumuli.

Pamoja Tujenge Uchumi,



**Edson Rugaimukamu,**  
**MENEJA MKUU.**

Nakala: Mrajis wa Vyama vya Ushirika (T)  
Tume ya Maendeleo ya Ushirika  
S.L.P. 201,  
**DODOMA.** - Kwa taarifa.

Katibu Tawala (M),  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P 299,  
**BUKOBA.** - Kwa taarifa

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika (M)  
S.L.P. 299,  
**BUKOBA.** - Kwa taarifa

Katibu Tawala (W),  
**BUKOBA, MULEBA NA MISSENYI** - Kwa taarifa

Wakurugenzi Watendaji (W)



**BUKOBA, MULEBA NA MISSENYI** - Kwa taarifa

Mkurugenzi Mtendaji,  
Manispaa ya Bukoba,  
S.L.P. 284,

**BUKOBA.** - Kwa taarifa

Maafisa Ushirika (W),

**BUKOBA, MULEBA, MISSENYI NA MANISPAA YA MJI BUKOBA**

- Kwa taarifa